


# Nyani na mamba

- Hadithi kutoka Sri lanka



# Apen og krokodillen

- En fortelling fra Sri Lanka



Det var en gang, langt inne i en jungel på Sri Lanka.

I jungelen var det mange trær og mellom trærne rant det en bred elv.

Her bodde det en apeunge sammen med mammaen sin.

Han var søt, liten og brun med to svære ører og et stort hjerte.

Hapo zamani za kale, ndani ya msitu nchini Sri lanka, kulikuwa na miti mingi na mto mpana. Hapo alikuwa anaishi nyani pamoja na mama yake. Nyani alikuwa mkarimu, mdogo wa rangi ya kahawia mwenye masikio makubwa mawili na moyo mmoja mkubwa.



Hver dag klatret apeungen oppover trestammene. Han slang seg fra tre til tre, helt til han kom til elven.

Da sklei han ned trestammen og satte seg ved elvekanten, helt alene. Apeungen hadde ingen venner.

De andre dyrene ville ikke leke med ham.

De var mye eldre og løp raskere enn ham, så apeungen klarte ikke å ta dem igjen.

Kila siku mtoto wa nyani alikuwa anapanda juu na kuruka kutoka shina la mti mmoja hadi mti mwingine mpaka anafika katika kingo (pembezeni) mwa mto. Hapo huwa anashuka chini ya shina la mti na kukaa katika kingo (pembezeni) ya mto peke yake. Mtoto wa nyani hakuwa na marafiki. Wanyama wengine walikuwa hawachezi na yeye. Walikuwa ni wakubwa kwa umri na wenye kukimbia kwa kasi (haraka) kuliko yeye, hivyo mtoto wa nyani hakuweza kuungana nao tena.



Om kveldene dro han hjem til mammaen sin og la seg i fanget hennes. «Jeg har ingen venner å leke med,» pleide han å si. «Ikke vær lei deg barnet mitt.

Når du blir stor, kommer du til å få deg mange venner,» svarte mammaen. «Men jeg vil ha venner nå!» sa apeungen. «Jeg er din venn,» svarte mammaen. «Zzzz» ... og apeungen sovnet.


Jioni ilipofika alikuwa akirudi nyumbani kwao na kukaa na mama yake na kuanza kulia, “mimi sina marafiki wa kucheza nao” alikuwa akipenda kusema hivi. “usiseme hivyo mwanangu”. Hapo utakapokuwa mkubwa utakuja pata marafiki wengi”. Alijibu mama yake. “Lakini mimi ninataka kuwa na marafiki sasa hivi”. Alisema mtoto wa nyani”. “Mimi ni rafiki yako”, Mama yake alijibu. (Zzzz).... na mtoto wa nyani alikuwa amelala.



En dag da apeungen var ved elven, så han plutselig to svære runde øyne som stakk opp fra vannet.

Øynene svømte nærmere og nærmere.

Siku moja mtoto wa nyani akiwa katika kingo (pembezeni) za mto, aliona macho mawili makubwa yakiwa juu ya maji. Macho yalikuwa yakimsogelea kwa karibu na karibu zaidi ya sehemu alipokuwepo.



Plutselig var det et svært hode som stakk opp og sprutet masse vann på apeungen, slik at han ble klissvåt.

Det var et svært dyr med lang grønn snute, skarpe tenner og lang hale som kom opp av vannet.

Ghafila kulikuwa na kichwa kikubwa kimechomoza juu ya maji na kummwagia maji mengi mtoto wa nyani, hivyo akawa amelowana. Alitoka ndani ya maji, mnyama mkubwa mwenye pua ndefu ya rangi ya kijani, meno makali na shingo ndefu.

«Hvem er du?» spurte apeungen mens han rista av seg vannet. «Eh ... jeg ... jeg er en krokodille,» svarte dyret. «Og jeg er en ape. Skal vi være venner? Bestevenner?» spurte apeungen. «Venner, eh hva er det?» spurte krokodillen.

«Det betyr at vi skal leke sammen og ta vare på hverandre,» forklarte apen.

«Ok da, vi kan være venner, eh... bestevenner,» svarte krokodillen.



“Wewe ni nani?” aliuliza mtoto wa nyani wakati akijikung’uta maji mwilini mwake “Eh...mimi...mimi ni mamba” alijibu mnyama yule. “na mimi ni nyani”. tunaweza kuwa marafiki? Marafiki wakubwa?” Aliliuliza mtoto wa nyani. “Marafiki! eh ndio nini?”, aliuliza mamba. “Inamaanisha tutacheza pamoja na kutunzana kwa kila mmoja wetu.” alielezea mtoto wa nyani. “sawa tutakuwa marafiki”, eh... marafiki wakubwa” alijibu mamba.



Og så lekte de sammen:

Virre-virre- vapp, min venn har kommet

Virre-virre- vapp, hvor kom han fra

Virre-virre- vapp, han kom fra vannet

Virre-virre- vapp, det var da bra

Na wakacheza pamoja:

virre-virre vapp, rafiki yangu amekuja

virre-virre-vapp, ametoka wapi

virre-virre-vapp, ametoka kwenye maji

virre- virre- vapp, hivyo ni vizuri





Om kvelden tok de farvel  
og lovte hverandre å  
møtes dagen etter.

Jioni waliagana na  
kuahidiana kuonana siku  
inayofuata.

Så løp apen hjem til mammaen sin og sa: «Jeg har fått en venn». «Oi, så koselig», svarte mammaen glad.

«Han heter, han heter ... ko ... ko ...» «Kattepus?» spurte mammaen. «Nei,» svarte apeungen.

«Kanin?» spurte mammaen ivrig. «Nei, svarte apeungen. «Ku?» fortsatte mammaen. «Nei, han heter ko, ko, kokodille!», sa apeungen.

«KROKODILLE!» skrek apemammaen. «Krokodiller er farlige! De spiser andre dyr. De spiser aper! Du får ikke lov til å leke med krokodillen.»



Mtoto wa nyani alikimbia kwa mama yake na kumuambia: “Mimi nimepata rafiki”. Ah!, ni jambo zuri sana” alijibu mama yake kwa furaha.

“ Anaitwa, anaitwa... ma..ma..”

“paka/ nyau?” akauliza mama yake.

“Hapana” alijibu mtoto wa nyani.

“Sungura?” Aliuliza mama yake huku akiwa na shahuku.

“Hapana!” Alijibu mtoto wa nyani. “Ng’ombe ” aliendelea mama yake. “Hapana”, anaitwa ma, ma, mamba) alisema mtoto wa nyani

“MAMBA” Alipayuka mama yake nyani.

“Mamba ni hatari! Wanakula wanyama wengine. Wanakula nyani! hauruhusiwi kucheza na mamba”



Apeungen ble kjempe lei seg. Han hadde nettopp fått seg en venn.

Om kvelden, da han hadde lagt seg, klarte han ikke å sove. Plutselig kom han på en idé:

Mtoto wa nyani alilia sana. Alikuwa ametoka kupata rafiki. Jioni hakuweza kulala, akiwa amelala, ghafla alipata wazo.




Dagen etter, plukka han bananer og tok med seg til krokodillen.

Siku iliyofuata alichuma mkungu wa ndizi na kwenda nao kwa mamba.

Apeungen ga bananene til krokodillen og sa: «Se, her har du litt frukt. Det smaker kjempegodt.» Krokodillen spiste litt av banan og sa «Eh ... ja, kjempegodt». «Jeg skal hente frukt til deg hver dag,» sa apeungen. «Men da må du love at du aldri mer spiser andre dyr.» «Eh ... ok da,» lovet krokodillen.

Mtoto wa nyani akampatia mamba ndizi na kusema “ona, hapa umepata matunda kidogo” Mamba akala kidogo zile ndizi na kusema “Eh...ndio, nzuri sana”. “Mimi nitakuwa nakuletea matunda kila siku” alisema mtoto wa nyani “lakini inabidi unihaidi kuwa kamwe hutakuwa unakula tena wanyama wengine” “Eh... sawa” Alihaidi mamba.





Hver dag, kom apeungen med et fruktfat til krokodillen, med alle mulig frukter, deilige frukter: bananer, ananas, kiwi, klementiner, mango. Så lekte de og hadde det kjempemoro sammen.

Når det ble kveld dro apen hjem til mammaen sin, mens krokodillen satte fruktfatet på ryggen, svømte hjem til kona og delte frukten med henne.

Kila siku, akawa anakwenda mtoto wa nyani na kapu la matunda kwa Mamba, matunda yote yanayoweza patikana, matunda matamu sana: ndizi, nanasi, kiwi, chenza, embe.

Hivyo wakawa wanacheza na kufurahi sana pamoja. Inapofika jioni mtoto wa nyani anarudi nyumbani, mamba yeye anabeba kapu la matunda mgongoni na kuogelea kuelekea nyumbani kwa mke wake na kugawana nae matunda.

En dag sa krokodillekona: «Frukten smaker godt, men det er noe som mangler.

Et apehjerte! Det hadde vært så godt å spise et lite apehjerte til frukten,» sa krokodillekona og ba mannen sin om å invitere apeungen hjem til dem, så de kunne spise hjertet hans. «Eh ... Men han er min venn,» sa krokodillemannen.

«En venn? Hva er det? Har aldri hørt om det,» svarte krokodillekona. «Har du glemt at vi krokodiller spiser dyr?» Hun ba mannen skynde seg, for hun var kjempesulten.



Siku moja mke wa mamba alisema “matunda yana ladha nzuri, lakini kuna kitu kinakosekana. Moyo wa nyani! Itakuwa vizuri sana kula moyo mdogo wa nyani pamoja na matunda” alisema mke wa mamba, na alimuomba mume wake amualike mtoto wa nyani nyumbani kwao ili aweze kula moyo wake “eh...lakini yeye ni rafiki yangu” alisema mume wake mamba. “Rafiki? ni nini hicho? Sijawahi sikia kitu kama hicho” alijibu mke wa mamba “umesahau kuwa sisi mamba tunakula wanyama wengine”, Mke wa mamba alimsisitiza aharakishe kwenda kumchukua mtoto wa nyani kwani alikuwa na njaa kali.



Krokodillen svømte til apen og inviterte ham hjem til middag.

Apen ble kjempeglad, men så kom han på en ting:

«Jeg kan jo ikke svømme», sa apeungen. «Hvordan skal jeg bli med deg hjem?»

Mamba aliogelea mpaka kwa nyani na kumualika nyumbani kwake kwa chakula cha jioni. Nyani alifurahi sana, ila akaja jua kitu kimoja “Mimi siwezi kuogelea”, alisema mtoto wa nyani. “Jinsi gani mimi nitakuja nyumbani kwako?”.





«Eh ... Du kan sette deg på ryggen min,» sa krokodillen.

Det syntes apen var en god ide. Så han hoppa opp på ryggen til krokodillen, og sammen dro de hjem til krokodillekona.

“Eh... Unaweza kukaa juu ya mgongo wangu” alisema mamba. Nyani alifikiria, hili ni wazo zuri. Hivyo akaruka juu ya mgongo wa mamba, wote kwa pamoja wakaelekea nyumbani kwa mke wa mamba.



Da de nærmet seg huset til krokodillen, stod krokodillekona ved elvekanten, hun hadde på seg et kjøkkenforkle og holdt en stor gaffel i hånda, klar for å spise opp apeungen.

«Eh ... Du skjønner, kona mi hadde lyst på et apeherte. Så jeg tok deg med hit slik at hun kunne spise deg opp,» sa krokodillen.

Wakiwa wanakaribia nyumbani kwa mamba, alikuwa amesimama mke wa mamba katika kingo(pembezeni) mwa mto, alikuwa amevalia kitambaa cha jikoni na ameshika uma mkubwa mkononi, tayari kwa kumla mtoto wa nyani. “Eh... unajua, mke wangu anahamu ya kula moyo wa nyani. Hivyo nimekuleta hapa ili aweze kukula” alisema mamba.



«Jeg har glemt igjen hjertet mitt,» sa apen.

«Eh ... Hva mener du?»


«Du skjønner ...» svarte apen. «Hjertet mitt hadde blitt vått, så jeg tok det ut og la det til tork.

“Mimi nimeusahau tena moyo wangu” alisema nyani.

“Eh... unamaanisha nini?”

“Unajua..” alijibu nyani.

“Moyo wangu ungelowana, sasa nimeutoa nje na kuuweka sehemu kavu”.



Det henger i det store treet ved elva.» Krokodillen skjønnte ingenting «Eh ... Hva skal vi gjøre nå? Kona mi kommer til å kjeft på meg!» sa krokodillen

Unaning'inia katika mti ule mkubwa pembeni ya mto. Mamba alikuwa hajui kitu chochote "Eh... sasa tutafanya nini?"

Mke wangu atakuja nikalipia mimi!", Alisema mamba



«Vi må svømme tilbake og hente hjerte mitt,»  
svarte apeungen.

«God ide,» sa krokodillen og svømte tilbake med apeungen på ryggen.

“Inabidi tuogelea turudi kuuchukua moyo kwenye mti” alijibu mtoto wa nyani.

“Wazo zuri ” alisema mamba na kurudi kwa kuogelea akiwa amembeba mgongoni mtoto wa nyani.



Da de kom fram til det store treet, sa krokodillen til apen om at han måtte skynde seg.

Apeungen hoppet ned fra krokodillens rygg og klatret raskt opp i treet.

Dermed kunne ikke krokodillen få tak i ham lenger.

«Du er ikke min venn lenger,» sa apeungen og sprang hjem.

Walipofika mbele ya mti mkubwa, mamba alimwambia nyani haya harakisha. Mtoto wa nyani alishuka katika mgongo wa mamba na kupanda haraka juu ya mti. Kiasi ambacho mamba asingeweza kumshika tena. “wewe si rafiki yangu tena” alisema mtoto wa nyani na kukimbia nyumbani.



Han hoppet rett opp i fanget til mammaen sin og lovte at han, fra da av, skulle høre på mammaen sin og aldri mer bli venn med en krokodille.

Snipp snapp snute, så er eventyret ute.

Nyani aliruka mpaka kwa mama yake na kumuhaidi kuwa atakuwa ana msikiliza na kamwe hatakuwa rafiki na mamba.

Na hadithi yetu ndio inaishia hapa.



Illustratør: Svetlana Voronkova

Se flere fortellinger på [morsmal.no](http://morsmal.no)